TANGAZO LA SERIKALI NA. 522 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA KALAMBO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA YA KALAMBO


MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA KALAMBO

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 46539.739 au Kilometa za Mraba 465.397

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi iliyohifadhiwa awali chini ya Msitu wa Hifadhi wa Taifa Kalambo River lenye ukubwa wa takribani Hekta 45995.839 au Kilometa za Mraba 459.958 na Msitu wa Hifadhi wa Taifa Kalambo Fall lenye ukubwa wa takribani Hekta 543.9 au Kilometa za Mraba 5.439 linalopatikana Wilaya ya Kalambo, Mkoa wa Rukwa kama lilivyochorwa katika Ramani za Idara ya Upimaji Jb 2908 ya mwaka 2015 (Skeli 1:75,000) na Jb 346 ya mwaka 1957 (Skeli 1:10,000) mtawalia zilizohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na ambazo majira nukta yake yameainishwa katika Majedwali yalipo katika kila ramani zenye Jb 2908 na Jb 346 kama ifuatayo:


KALAMBO FALLS FOREST RESERVE
UFIPA DISTRICT WESTERN PROVINCE
Jb 346
Scale 1: 10,000




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*